

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



*Angola*  
*08 Aprili, 2025*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepongeza juhudi za Rais wa Jamhuri ya Angola, Mhe. João Manuel Gonçalves Lourenço kudumisha uhusiano na urafiki wa muda mrefu baina ya nchi hizi mbili na kuwa makubaliano yaliyofikiwa kwenye ziara yake nchini Angola yataenda kuimarisha uhusiano wa kiuchumi.

*“Kutokana na kuwepo kwa fursa nyingi katika nchi zetu mbili, ikiwemo kwenye sekta za Kilimo, Utalii, Viwanda na Uchumi wa Buluu, tumekubaliana kuimarisha mahusiano ya biashara na uwekezaji baina ya nchi zetu. Ni kwa msingi huo, tumeshuhudia utiaji saini wa Hati ya Makubaliano ya ushirikiano kati ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Angola Private Investment and Export Promotion Agency (AIPEX), ikiwa ni hatua muhimu ya kukuza kiwango cha uwekezaji baina ya nchi mbili hizi,”* amesema Rais Dkt. Samia.

Rais Dkt. Samia ametoa pongezi hizo leo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano wa pamoja na mwenyeji wake Mhe. Rais João Manuel Gonçalves Lourenço katika Ikulu ya nchi hiyo iliyopo Luanda.

Aidha, katika kumarisha zaidi ushirikiano uliopo baina ya watu wa Tanzania na Angola na kuzidi kukuza biashara na uwekezaji, Rais Dkt. Samia ametangaza kuwa Tanzania pia itaondoa sharti la kulipia visa ya utalii kwa raia wa Angola kuingia Tanzania, kama ambavyo Serikali ya Jamhuri ya Angola ilivyoondoa sharti hilo kwa raia wa Tanzania kuingia nchini humo tangu mwaka jana.

Kwa upande wake, pamoja na mambo mengine, Rais Lourenço ameridhia mwaliko wa Rais Dkt. Samia kufanya ziara nchini Tanzania mwezi Julai, 2026 ambapo mbali ya ziara hiyo



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



atakuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa kihistoria wa Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, yatakayoambatana na mkutano wa wafanyabiashara wa Tanzania na Angola.

Vilevile, leo Rais Dkt. Samia na mwenyeji wake Rais Lourenço wameshuhudia utiaji saini wa Mikataba ya ushirikiano katika masuala ya ulinzi pamoja na Hati ya makubaliano kuhusu kukuza Uwekezaji.

Awali, Rais Dkt. Samia alianza ziara yake kwa kutembelea Mnara wa Kumbukumbu katika Makumbusho ya António Agostinho Neto, Muasisi na Rais wa Kwanza wa Angola, ambapo aliweka shada la maua na kutoa heshima katika kaburi la muasisi huyo.

Katika hatua nyingine, kufuatia mwaliko wa Mhe. Carolina Cerqueira, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Angola, Rais Dkt. Samia amelihutubia Bunge hilo, ambapo pamoja na mambo mengine amesema kuwa nchi za Afrika zinatakiwa kupambana katika vita ya uchumi kwa moyo uleule ambao waasisi wa mataifa ya Angola na Tanzania walivyopambana kuzikomboa nchi zao kutoka kwenye ukoloni.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Tanzania na Angola zimekubaliana kuunganisha nguvu katika kuongeza fursa za kiuchumi kwa watu wa nchi hizi, hususan vijana. Katika kuimarisha mahusiano haya, Rais Dkt. Samia ametangaza kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakusudia kufungua upya Ubalozi wake nchini Angola.

Sharifa B. Nyanga  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU



*Ikulu Mawasiliano / ikulu\_mawasiliano /  
ikulu\_Tanzania / ikulu Tanzania /  
ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

